
# UFUGAJI BORA WA NGURUWE



**Mwongozo wa ufugaji bora wa nguruwe kwa mfugaji mdogo, kuzingatia tija, afya na thamani ya mnyama**

Umetolewa na Mradi wa SLIPP wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Morogoro, Tanzania kupitia Ufadhili wa DANIDA

Watayarishaji:
Profesa Faustine P. Lekule
Profesa Amandus Muhairwa
Dr. Helena Ngowi
Dr. Daniel Mushi
Dr. Eliakunda Casmir Kimbi

Mchoraji
Simon John Rwegayura

## 1. Utangulizi

Ufugaji wa Nguruwe ni kati ya shughuli zinazokuwa haraka katika Afrika Mashariki na ya Kusini. Ukuaji wa miji na ongezeko la watu kumeendana na ongezeko kubwa la mahitaji ya protini ya wanyama. Uwezo wa kukua haraka, ubora wa nyama kiafya na ladha nzuri inatoa nafasi kubwa ya maendeleo ya ufugaji wa nguruwe kama chanzo cha kipato kwa mfugaji. Kijarida hiki kinatoa mwongozo kuhusu mahitaji muhimu ya ufugaji nguruwe, mbinu za kuboresha uzalishaji, kudhibiti magonjwa na pia mwongozo wa kujali haki za nguruwe kama kiumbe hai kinachoweza kusikia maumivu kisipotendewa kinavyostahili. Nguruwe ana gharama ndogo za matunzo, anatoa mafuta, huleta kipato cha pesa, hutoa mbolea ya mimea. Faida ya ufugaji nguruwe hutegemea zaidi ubora wa matunzo. Vile vile kumbuka kutumia vyanzo nafuu vya chakula na kujengea miudombinu. Msomaji anashauriwa kuwaona wataalamu kwa ushauri zaidi na pia kusoma vitabu vya rejea kuhusu ufugaji nguruwe.

## 2. Ukweli kuhusu Nguruwe

Nguruwe ni mnyama msafi sana na mwenye akili. Akipewa banda lenye nafasi ya kutosha huweza kuchagua sehemu ya kulala, kujisaidia na akauweka mwili wake katika hali ya usafi sana. Usafi wa banda na mazingira utakuhakikishia nguruwe wasafi bila uchafuzi wa mazingira kama tunavyoona kwa wafugaji wengi mijini na vijijini. Tenga mavazi na viatu maalumu kwa ajili ya kazi za nguruwe na oga vizuri baada ya kufanya kazi kwenye mabanda ya nguruwe kwa muda mrefu.

## 3. Nyumba ya nguruwe

Kwa ujumla nyumba za aina mbili huhitajika katika ufugaji wa nguruwe


- o Nyumba za kukuzia na kunenepesha nguruwe wa kuchinja
- o Nyumba za nguruwe wazazi


### Sifa za msingi za nyumba bora ya nguruwe

- Nyumba ijengwe eneo lenye kivuli cha kutosha
- Nyumba iwe na nafasi ya kutosha
- Ijengwe sehemu yenye mwinuko kiasi ili kuwezesha maji kuondoka kwa urahisi
- Iwe na chombo/kihori cha kuweka chakula na kingine chakuweka maji
- Iwe na sakafu imara iliyotengenezwa kwa saruji, mabanzi, miti na isiwe na unyevu
  - Sakafu ya saruji iwe na mteremko (slope) inayoweza kuondoa uchafu kwa urahisi ndani ya banda.
  - Sakafu ya mabanzi, mbao au miti iwe inatoa nafasi ya kuondoa uchafu kama kinyesi ndani ya banda.
- Iwe na mtaro wa kuondolea maji, mkojo na kinyesi hadi shimo la kutunzia
- Kuta za mabanda ya nguruwe zinatakiwa kuwa imara, ziwe na uwezo wa kuwasitiri nguruwe wasitoke nje.

▪ Iweze kuingiza hewa ya kutosha ndani ya banda hasa kama ukuta umezibwa (solid walls)


- Paa linaweza kupauliwa vizuri kwa nyasi, makuti, bati n.k kama inavyoonekana hapa chini




*Mabanda kwa ajili ya nguruwe wanne wenye umri wa miezi minne hadi mitano. Vipimo vya banda: 2 x 2.5 m. Zingata vipimo vilivyoonyeshwa ili kuruhusu hewa kupita na kuwapa nguruwe nafasi ya kutosha*

Banda hili hapa chini limejengwa kwa ajili ya mama nguruwe na watoto. Vipimo: ukubwa wa banda = 2 x 2 m, ukubwa wa sehemu ya mama nguruwe = 0.6 x 0.6, sehemu ya watoto = 0.6 x 0.6 m




## 4. Upate wapi Nguruwe wa Kufuga

Nunua nguruwe wa kufuga kutoka kwenye mashamba au wafugaji wanaoaminika ukizingatia yafuatayo.

- Usizalishe nguruwe wanaotokana na ukoo mmoja yaani ndugu kama kaka na dada. Nunua dume na jike toka mahali tofauti.
- Tumia ushauri wa wataalamu kuchagua nguruwe bora

Sifa za kuangalia kwa nguruwe bora wa mbegu:

- Nguruwe wa mbegu awe na sifa ya kukua haraka na asiwe na ulemavu wa aina yeyote, na hasa wa miguu kwa dume.
- Mama mzazi wa nguruwe awe na historia ya kuzaa watoto 10 hadi 12 kwa mzao mmoja
- Jike awe na chuchu zaidi ya 12.
- Dume awe na sehemu za kiume yaani korodani na uume unaoonekana sawa sawa. Pia awe na hamu ya kupanda majike.

## 5. Mbinu za uzalishaji

### Matunzo ya dume la uzalishaji

- Chagua dume la mbegu bora, lisilokuwa na kilema au ugonjwa wowote. Tenganisha dume na majike ili kuepusha kupandwa kusiko na kumbukumbu. Dume la nguruwe halipaswi kunenepa, kwa hiyo usimlishe chakula kingi na mpatie mazoezi ya kutosha asije akawa mvivu
- Nguruwe dume anaanza kupanda majike akiwa na umri wa miezi 4 hadi miezi 9. Dume liruhusiwe kupanda mara moja tu kwa kila juma. Anapofika miezi 10 anaweza kupanda mara mbili hadi mara tatu kwa wiki. Akiwa na mwaka mmoja na zaidi anaweza kupanda kila siku kwa majuma mawili hadi matatu, kisha apumzike kwa majuma mawili. Ni vizuri nguruwe dume mmoja apande majike 15 hadi 20 kwa mwaka.
- Madume madogo yapande majike madogo, dume kubwa likimpanda jike dogo anaweza akamletea maradhi ya mgongo. Ni muhimu kupandisha dume kabla hajala chakula, na asitumiwe mara tu baada ya chakula ili asiwe mvivu.

### Utunzaji nguruwe mwenye mimba

- Mimba ya nguruwe huchukuwa miezi mitatu (3) wiki tatu(3) na siku tatu(3) yaani siku 114
- Nguruwe mwenye mimba apewe chakula cha kutosha kiongezwe polepole tokea posho ya kawaida hadi kilo 3 – 3.5 kwa siku.

### Matayarisho ya nyumba kabla ya kuzaa

- Osha banda la kuzalia kwa maji na kuliacha likauke
- Tandika nyasi kavu mara baada ya nyumba kukauka
- Ongeza taa ya chemli au umeme kama uko mikoa yenye baridi kwenye sehemu ya vitoto.
- Tengeneza sehemu ya kuzalia kwa mbao au mabomba (Tazama picha namba 3)

### Kumuandaa nguruwe mama kabla ya kuzaa

- Mpe dawa ya minyoo siku 10 kabla ya kuzaa
- Mogeshe mama nguruwe kwa sabuni ya mkono na brashi
- Muhamishie katika chumba cha kuzalia siku 7 kabla hajazaa
- Mpunguzie lishe siku 2 kabla ya kuzaa
- Siku ya kuzaa mpe nguruwe maji ya kunywa tu

### Matunzo ya vitoto vya nguruwe

Vitoto vya nguruwe vinyonye maziwa ya mama siku zote hadi wakifikisha siku 56. Mambo muhimu ya kufanya kwa vitoto vya nguruwe yameainishwa kwenye jedwali namba 1 hapa chini:

***Jedwali namba 1: Mambo muhimu ya kufanya kwa vitoto vya nguruwe***

| SIKU | JAMBO LA KUFANYA |
|---|---|
| 1 | • Kata vitovu virefu kwa wembe mpya au mkasi uliochemshwa<br>• Nyunyuzia Iodine katika vitovu<br>• Kata meno makali juu na chini<br>• Mpe mama nguruwe chakula kidogo kama nusu kilo |
| 3 | • Vitoto vya nguruwe vipewe sindano ya madini ya chuma<br>• Viwekewe maji safi ya kunywa |
| 5 | • Ongeza chakula cha mama hadi kufikia kilo mbili na nusu |
| 10 | • Viwekee alama (identification) vitoto vya nguruwe<br>• Hakikisha makaazi ya nguruwe ni masafi na mpe mama kilo sita(6) za chakula. |

## Upandishaji jike

- Kati ya siku nne hadi saba baada ya kuachishwa watoto, nguruwe mama hupata joto. Nguruwe jike alie kwenye joto apelekwe kwenye banda la dume na sio kinyume chake. Rudia kumpandisha jike alie kwenye joto masaa 12 baada ya mpando wa kwanza; rudia kumpandisha mara 2 hadi 4. Kama jike hatarudia kwenye joto baada ya wiki 3 atakuwa ameshika mimba.

## Dalili za joto

- Sehemu ya uzazi kubadilika na kuwa nyekundu
- Nguruwe hatulii na hukojoa mara kwa mara
- Ute kama makamasi hutoka sehemu za siri
- Nguruwe mwenye joto hujaribu kuwapanda wenzake na yeye akipandwa hutulia

# 6. UTUNZAJI WA VITOTO VYA NGURUWE.

## Ulishaji wa maziwa ya kwanza

Baada ya kuzaliwa na kusafishwa, hakikisha vitoto vinanyonyeshwa. Vitovu viwekewe dawa (Iodine 5%) ili kuzuia magonjwa. Kama mama amefariki mara tu baada ya kuzaa na hakuna nguruwe mwingine anayeweza kunyonyesha; tumia maziwa ya ng'ombe, ongeza sukari na yai bichi koroga na uwanyonyeshe kwa kutumia chupa ya maziwa ya mtoto.

## Joto


Vitoto vya nguruwe havizaliwi na manyoya na hawana mafuta mengi ya kutosha kuwaletea joto mwilini; hivyo ni rahisi kufa kwa baridi. Tumia taa ya stimu au chemli kuongeza joto.

## Kuzuia upungufu wa damu

Maziwa ya nguruwe yana upungufu wa madini ya chuma yaongezayo damu. Hivyo baada ya majuma mawili au matatu watoto huanza kudhoofu kwa kukosa madini hayo mwilini. Kuondoa tatizo hili inabidi vitoto vidungwe sindano ya madini kwenye misuli siku mbili au tatu tangu kuzaliwa. Kama sindano haipatikani njia nyingine za kuwapatia watoto madini hayo ni kwa kuwapa vidonge vya madini chuma, au kuwapa madini hayo kwenye ndimi zao au chuchu za mama yao siku mbila hadi tatu baada ya kuzaliwa.

## Ukataji meno

Siku chache kabla ya kuzaliwa, meno yaliochongoka kama sindano huchomoza katika taya mbili. Meno hayo humuumiza mama wakati watoto wanapo nyonya, matokeo yake mama hupiga watoto mateke. Hii husababisha vifo vya watoto kutokana na kupigwa na kukosa maziwa ya mwanzo. Hiyo inabidi meno hayo yakatwe na chombo kinachofanana na mkasi (Tazama picha namba 4), ili kupunguza madhara hayo. Muone bwana mifugo kwa maelezo zaidi.



*Picha namba 4*

### Kulisha chakula cha ziada

Chakula kigumu zaidi ya maziwa kianze kulishwa kidogo kidogo kuanzia siku ya kumi baada ya kuzaliwa, kwani wakati huu maziwa ya mama hayatoshelezi. Endelea kuwapa chakula hiki mpaka watakapo zoea kutokunywa maziwa ya mama yao tena. Chakula hiki kiwe na viini lishe vya kujenga mwili, kuleta nguvu na kuzui maradhi. Nguruwe wapewe chakula hiki kwa wingi na maji ya kutosha.

### Kuhasi

Vitoto ambavyo havihitajiki kwa ajili ya kizazi bora katika mfugo, vihasiwe vikiwa katika juma la tatu hadi la nne. Nguruwe walio hasiwa huwa wapole, wenye nguvu, wazito na nyama yao haina harufu ya dume. Bwana mifugo atakupa maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kufanya.

### Kuachisha kunyonyesha

- Viachishe vitoto kunyonya wakifikia umri wa miezi miwili wanapokuwa na uzito wa kilo 10.
- Siku ya kuachisha kunyoyesha muondoe mama nguruwe kwa watoto wake na kumuweka chumba kingine
- Mpe mama chakula cha kutosha

## 7. Vyakula na ulishaji

Chakula bora kwa nguruwe ni moja ya mahitaji muhimu sana kwenye dhana nzima ya ufugaji wa nguruwe wenye tija na faida kwa mfugaji. Chakula cha nguruwe kinagharimu yapata asilimia hamsini sabini ya gharama zote za ufugaji wa nguruwe. Kati ya matatizo mengi yanayosababisha tija na ufanisi duni wa uzalishaji wa nguruwe yanatokana na lishe duni. Nguruwe wakipatiwa lishe bora, tija na ufanisi wa uzalishaji utakuwa mkubwa hivyo kuongeza faida kwa mfugaji.

**B. Baadhi ya faida za lishe bora kwa nguruwe ni:**

1. Lishe bora huharakisha ukuaji wa haraka wa nguruwe na hivyo kupata uzito unaohitajika kwa kipindi kifupi.
2. Lishe bora hupunguza gharama za ufugaji na hivyo kuongeza faida kwa mfugaji kwa sababu nguruwe atahitaji kiasi kidogo tu cha chakula na atachukua muda mfupi kupata uzito mkubwa
3. Lishe bora itapunguza maambukizi ya magonjwa.
4. Lishe bora huongeza kiasi cha mayai yatakayoivishwa na mama nguruwe na hivyo kuongeza idadi ya watoto watakaozaliwa
5. Lishe bora huongeza kiasi cha maziwa yatakayotengenezwa na mama nguruwe kwa ajili ya watoto hivyo kuwafanya wawe na afya bora itakayo wawezesha wakue haraka na kupunguza idadi ya vifo kwa watoto.
6. Lishe bora inaongeza ufanisi wa madume ya nguruwe na hivyo kuongeza uwezo wa kupanda

**C. Viini lishe muhimu kwenye lishe ya nguruwe**

Nguruwe wana uwezo wa kula aina nyingi za vyakula lakini vyenye uwezo wa kumeng'enywa kwa urahisi. Chakula cha nguruwe kilichokamilika kinahitaji kuwa na mchanganyiko wa viini lishe vitano, navyo ni

1. Vyakula vyenye kutia nguvu mwilini (kama pumba za mahindi, ngano, mchele)
2. Vyakula vya kujenga mwili (kama mashudu ya alizeti, pamba, unga wa dagaa)
3. Vyakula vya asili ya madini (kama chumvi, chokaa, mifupa iliosagwa)
4. Vyakula vya asili ya vitamini (kama majani mabichi, mbogamboga na matunda)
5. Maji

## D. Jinsi ya kutengeneza chakula cha nguruwe

Wakati wa kutengeneza chakula cha nguruwe inabidi kuzingatia yafuatayo:

- Mchanganyiko wake uwe na viinilishe vinne vilivyotajwa hapo juu
- Chagua aina ya viinilishe vinavyoweza kupatikana kwa urahisi na bei nafuu kwenye mazingira yako
- Aina ya mchanganyiko wa chakula ni muhimu uzingatie mahitaji ya nguruwe kama umri (mfano: nguruwe wanaonyonya, waliochishwa kunyonya, wanaokua, na wanaonyonyesha)

Mfano jedwali Na 2 linaonyesha michanganyiko mbalimbali ya vyakula vya nguruwe.

1. *Mchanganyiko **namba 1***: inapendekezwa kwa wafugaji walioko kwenye mazingira ambayo pumba za mahindi na mashudu ya alizeti yanapatikana kwa urahisi
2. *Mchanganyiko **namba 2***: kwa wale ambao pumba za mahindi, za mpunga machicha ya pombe na mashudu ya alizeti yanapatikana kwa urahisi.
3. *Mchanganyiko **namba 3***: kwa wale ambao pumba za mpunga na mahindi yanapatikana kwa urahisi.

**Jedwali namba 2: Michanganyiko mbalimbali ya vyakula vya nguruwe**

| Na | Aina ya viinilishe | Michanganyiko | (Asilimia) | |
|---|---|---|---|---|
| | | Namba 1 | Namba 2 | Namba 4 |
| 1 | **Vyakula vya wanga** | | | |
| | 1. Pumba za mahindi | 70.25 | 32 | 30.00 |
| | 2. Pumba laini za mpunga | - | 25 | 33.00 |
| | 3. Machicha ya pombe yaliyokaushwa | - | 21 | - |
| | 4. Mahindi yaliyobarazwa | | | 10.00 |
| 2 | **Vyakula vya protini** | | | |
| | ***A. Protini ya nafaka*** | | | |
| | 1. Mashudu ya alizeti | 22.00 | 14 | 22.00 |
| | 2.Mashudu ya michikichi | - | - | |
| | 3. Soya iliyochemswa na kubarazwa | - | - | - |
| | ***B. Protini ya Wanyama*** | | | |
| | 4.Unga wa dagaa/samaki | 4.00 | 2.00 | 3.25 |
| | 5.Damu iliyokaushwa | - | 2.25 | - |
| 3 | **Vyakula vya asili vya madini** | | | |
| | 1. Chumvi ya mezani | 0.50 | 0.50 | 0.50 |
| | 2. Chokaa ya mifugo | 2.00 | 2.00 | 2.00 |
| | 3. Unga wa mifupa | 1.00 | 1.00 | 1.00 |
| | 4. Madini na vitamini mchanganyiko | 0.25 | 0.25 | 0.25 |
| | Jumla | 100. | 100 | 100. |

E. **Kiasi na namna ya kulisha**

- Nguruwe wanahitajika kulishwa aina hii ya chakula mara mbili (asubuhi na mchana) au zaidi kwa siku
- Kiwango/kiasi cha kulisha kwa nguruwe wa aina na rika tofauti kimeonyeshwa kwenye jedwali Namba 3
- Pamoja na vyakula vilivyotajwa, wafugaji wanashauriwa kuwapatia nguruwe vyakula vyao vya kijadi kama vyakula vya ziada mfano, majani mabichi laini, majani ya maboga, mbogamboga, matunda kama maparachichi, majani ya viazi n.k.

Jedwali na 3: Viwango vya kulisha nguruwe wa uzito mbalimbali

| Na | Wakati | Uzito wa nguruwe (kilo) | Kiasi cha chakula (kilo kwa siku) |
|---|---|---|---|
| 1. | Baada ya kuachishwa kunyonya hadi uzito kiasi | 10 - 17 | 0.75 |
| 2. | Uzito uliozidi kiasi kidogo | 18 - 29 | 1.00 |
| 3. | Uzito wa kawaida | 30 - 40 | 1.50 |
| 4. | Uzito mkubwa kiasi | 41 - 60 | 2.00 |
| 5. | Uzito mkubwa | 61 - 80 | 2.5 |
| 6. | Uzito mkubwa sana | 81 – 100 | 3.00 |
| 7. | Nguruwe anaye nyonyesha | 120 – 150 | 6.00 |

**Jinsi ya kulisha jike la nguruwe kabla na baada ya kuzaa**

1. Kipindi cha mimba, kuzaa hadi kuachisha kunyoyesha

1.1 Kipindi cha miezi mitatu baada ya kupandishwa

- Apatiwe chakula kiasi kama kilo mbili kwa siku
- Kiasi hiki kiendelee hadi wiki 3 kabla ya kuzaa

1.2 Wiki tatu kabla ya kuzaa

- Ongeza chakula kufikia kilo mbili na nusu.

1.3 Wiki moja kabla ya kuzaa

- Anza kuopunguza chakula taratibu hasa vyakula vya nafaka (Concentrate rations).
- Ongeza vyakula vya mbogamboga, majani laini na matunda (laxative meals).

1.4 Siku ya kuzaa

- Usimpe chakula chochote cha nafaka.
- Mpe vyakula vya mbogamboga,na vilaini kwa kiasi kidogo tu
- Mpatie maji ya kutosha.

1.5 Siku ya 1 – 2 baada ya kuzaa

- Mpe nusu kilo ya chakula kamilifu.

1.6 Siku ya 3 na kuendelea

- Ongeza chakula cha nafaka kwa kiasi cha kilo 1 kwa siku.
- Ongeza kufikia kiwango kinachohitajika kulingana na idadi ya watoto alionao mama nguruwe.

*Zingatia*

- Mama nguruwe anahitaji kilo 3 za chakula kwa matumizi yake ya kawaida.
- Atahitaji kiasi cha ziada cha theluthi moja (1/3) ya kilo ya chakula kwa kila mtoto aliyenae

*Mfano: kama mama ana watoto 9 atahitaji kiasi gani cha chakula?*

| Mahitaji mama peke yake | Mahitaji kutokana na watoto | Kiasi cha chakula kwa siku |
|---|---|---|
| 3kg | Theluthi moja x 9: ($^1/_3$ x 9 = 3 Kg) | 3 kg + 3 kg = Kilo 6 kwa siku |

- Endelea kumpa kiwango hicho cha chakula mpaka ifikapo wiki moja kabla ya kuwaachisha watoto kunyonya.
- Wiki moja kabla ya kuwachisha punguza kiwango taratibu mpaka kufikia kilo 3½ kwa siku.

**Baada ya kuachisha kunyonya**

- Mama nguruwe wapatiwe chakula bora kilicho na kiwango kikubwa cha madini na vitamini kiwango cha kilo 2 – 3 kwa siku.
- Hii itamsaidia kuivisha mayai, hivyo kumsaidia kupata joto mapema.

## 8. Magonjwa na Afya

Magonjwa yafuatayo ya nguruwe yameelezwa kifupi:-Ili kumpa mfugaji maarifa ya kutambua na kuzuia /kutibu. Waone wataalamu ukiona dalili hizi

| Dalili | Ugonjwa | Udhibiti/Tiba |
|---|---|---|
| Homa kali, kukosa raha na kuwa mkali kwa watoto | Ukosefu wa maziwa | Mama nguruwe atibiwe kwa antibiotiki kama na homa. Mtalamu akague chuchu kuona kama zina matatizo ya kuzaliwa. Kagua meno ya vichanga kama hayajakwatwa yakatwe. |
| Uharo wa njano nguruwe akiwa na umri wa wiki 3 | Kuhara kwa nguruwe wachanga | Tibu kwa antibiotiki. Safisha Banda, vyombo na mazingira kila mara kuua vimelea kwenye mazingira |
| Malengelenge ya mafua puani mdomoni, chuchu na kwato | Ugonjwa wa miguu na midomo | Ugonjwa hauna tiba maalumu. Osha vidonda kwa dawa ya kuua vimelea vya magonjwa. |
| Vifo vya ghafla damu puani na sehemu ya kutolea kinyesi | Kimeta | Toa taarifa haraka kwa mtaalamu aliye karibu, kwani nyama ya nguruwe hawa haifai kuliwa. |
| Kujikuna katika vizingiti na kuharibika ngozi | Ukurutu | Sindano ya Ivermectin kwa nguruwe wote. Rudia baada ya wiki 2 |
| Joto kali, vifo vingi sana kushindwa kutembea, kutokula. | Homa ya nguruwe | Hakuna dawa, toa ripoti kwa mtaalamu ili taratibu za udhibiti zifuatwe. |

# 9. Matunzo na udhibiti na haki za msingi

## Kushika na kuongoza nguruwe

Nguruwe anapaswa kuanza kushikwa tokea akiwa mdogo ili azoane vema na binadamu. Mfugaji anapaswa kujifunza jinsi ya kushika, kuongoza na kumuangusha nguruwe bila kusababisha maumivu au msongo kwa mnyama.




*Picha namba 5*

### 1. Kubeba nguruwe mtoto

Mkamate nguruwe mtoto kwa kukamata miguu ya nyuma, mnyanyue na kuweka mkono mwingine chini ya tumbo lake kama ilivyoonyeshwa kwenye picha. Hapo utaweza kumtibu, kumhamisha au hata kumkagua kama ana tatizo.

### 2. Kumuongoza nguruwe mkubwa

Kumuongoza nguruwe aende unapotaka inawezekana iwapo utatoa ubao wa kuongozea nguruwe. Ubao huo wenye upana sentimeta 80 na urefu wa sentimeta 80 unaweza kutengenezwa kwa kutumia mlango wa zamani au mbao za gharama ndogo. Mkinge nguruwe na ubao mmoja kila upande kulia na kushoto huku ukiacha nafasi ndogo ya kumruhusu kuona upande wa kichwani, fanya hivyo huku ukimuelekeza upande unaotaka aende. Unaweza kumuongoza nguruwe kwa ubao mmoja (picha na 6) iwapo kuna nafasi ya kumkinga kulia na kushoto kama ilivyoonyeshwa.



*Picha namba 6*

### 3. Kudhibiti nguruwe wakubwa



*Picha namba 7*

Tumia kamba ya katani iliyosukwa au waya wa kukamatia nguruwe (pig snare). Nguruwe akifungwa kamba ya kitanzi katika taya la juu la mdoma na kuvutwa kuelekea mbele, yeye atavuta kuelekea nyuma kama ilivyoonyeshwa katika picha namba 7, Mbinu hii huwezesha kumkagua nguruwe, kumchoma sindano, kumuogesha au hata kuruhusu kumfunga kamba miguuni ili kumuangusha.

### 4. Kumuangusha chini nguruwe

Kuangusha chini nguruwe, mfunge kamba mdomoni kama ilivyoonyeshwa hapo juu (Picha namba 8). Kisha funga miguu ya mbele pamoja kwa kamba moja, na miguu ya nyuma ifungwe kwa kamba nyingine. Mtu mmoja abakie kudhibiti kamba ya mdomoni ili nguruwe asitembee, mtu wa pili avute kamba za miguu moja moja huku akiwa amesimama (angalia picha) upande wa pili tokea zinapotokea kamba chini ya tumbo la nguruwe, Huyu avute zile kamba kila moja katika mkono tofauti, nguruwe ataanguka chini. Funga miguu vizuri kudhibiti nguruwe asiinuke.



*Picha namba 8*

### 10. Kulinda haki za nguruwe

a. Usimpige nguruwe kwa sababu yeyote ile
b. Usiwajaze nguruwe kwenye chumba kidogo kisicho na nafasi ya kutosha watapigana, watachafuka, na kuumizana
c. Usimuache nguruwe juani, nguruwe hatoki jasho joto litamtesa na hata kumuua
d. Usiweke madume wawili chumba kimoja hasa kama hawafahamiani, watapigana sana.
e. Usisafirishe nguruwe kwenye gari lisilo na nafasi ya kutosha na wasafirishaji jioni na asubuhi wakati hamna joto

**Fanya haya**

a. Wape nguruwe nafasi ya kutosha kama ilivyoelekezwa katika jarida hili.
b. Wape chakula na maji ya kunywa ya kutosha
c. Nguruwe akiugua apewe tiba mara moja ili kuepusha maumivu yasiyo ya lazima
d. Chinja nguruwe kwa taratibu zilizoelekezwa ili kumuepusha na kifo cha mateso